

SERA YA KUPINGA RUSHWA NA UFISADI

SERA

Perseus Mining Limited na kampuni zake tanzu (**Kampuni**), ni kampuni ya uchimbaji, uendelezaji na utafiti wa dhahabu inayofanya shughuli zake barani Afrika. Katika kuendesha shughuli zake, kampuni hairuhusu aina yoyote ya vitendo vya rushwa au ufisadi. Dhamira hii inatokana na msingi wa maadili yetu na inalenga kuimarisha utamaduni imara, wa uwazi na wa uadilifu, na uzingatiaji wa sheria, jambo ambalo ni muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu ya biashara yetu.

Wakurugenzi wote wa kampuni, wafanyakazi, wakandarasi, washauri na washirika wengine wa kibiashara pamoja na wafanyakazi wao, wanapaswa kufahamu na Kuzingatia sheria zote husika, na kupinga rushwa na ufisadi pamoja na sera hii. Kutokuzingatia hayo kunaweza kuiweka kampuni, wakurugenzi na wafanyakazi wake katika hatari ya adhabu kali za jinai au kesi za madai, pamoja na kuharibu sifa za kampuni.

Ili kutimiza dhamira hii, kampuni, Pamoja na mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya kampuni, lazima:

- Asitoe, asilipe, asiombe wala asikubali rushwa ya aina yoyote, iwe ni ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kutoka au kwenda kwa maafisa wa serikali, viongozi wa kampuni binafsi au mtu au taasisi yoyote.
- Aepuke viashiria vinavyoweza kuleta taswira ya kuonekana kana kwamba analipa au anapokea rushwa kupitia njia nyingine kama vile malipo ya kuwezesha shughuli (facilitation payments), michango ya kisiasa au burudani iliyokithiri, ukarimu au zawadi zisizo za kawaida au zilizopitiliza.
- Atunze kumbukumbu sahihi za kifedha pamoja na mifumo madhubuti ya udhibiti wa ndani.

Kampuni ina mfumo madhubuti wa kuziua, kugundua na kushughulikia mienendo mibaya, ikiwemo mafunzo, ukaguzi wa historia (background checks), mapitio ya usajili, ukaguzi wa ndani (audits), Pamoja na taratibu za uchunguzi wa utoaji wa taarifa.

Kwa maswali yoyote, tafadhali wasiliana kupitia: compliance@perseusmining.com

UTHIBITISHO NA MAPITIO

Sera hii itapitiwa kila mwaka.

TOLEO NA.	IMEANDALIWA NA/IMESASISHWA NA	IMEPITIWA NA	IMEPITISHWA NA	TAREHE	MAELEZO/ MABADILIKO YALIYOFANYIKA
2	Mwanasheria Mkuu na Katibu wa Kampuni	Kamati ya Ukaguzi na Hatari	Bodi	Februari 2026	Imepitiwa bila marekebisho